**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# MPANGO WA CHANJO NA UTAMBUZI WA MIFUGO KITAIFA (2024/2025 – 2028/2029)

**MEI 2025**



## DIBAJI

Tanzania ina rasilimali kubwa ya mifugo na ni nchi ya pili Barani Afrika kwa wingi wa mifugo. Pamoja na wingi wa rasilimali hizo mchango wake katika Pato la Taifa ni asilimia 6.2. Moja ya sababu za mchango huu kuwa mdogo ni pamoja na uwepo wa magonjwa ya mifugo yanayosababisha vifo na kuathiri biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi.

Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeandaa Mpango wa Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa kwa miaka mitano 2024/2025 – 2028/2029. Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi 216,140,097,000 kwa kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa mpango huu. Utekelezaji wa mpango huu utawezesha kuondoa vikwazo vya biashara za Kimataifa kwa nchi na kupata ithibati ya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH) na Shirika la Biashara Duniani (WTO), kuimarisha uzalishaji wa mifugo na mazao yake, kuimarisha afya ya jamii kwa kutokomeza magonjwa toka kwa wanyama kwenda kwa binadamu na kupunguza matumizi ya dawa yasiyo ya lazima ili kuondoa usugu wa vimelea dhidi ya dawa (UVIDA). Faida nyingine za mpango wa Chanjo na Utambuzi ni kuongeza uhakika na usalama wa chakula, kuongeza kipato kwa mfugaji na taifa, kuongeza biashara ya nyama nje ya nchi kutoka tani 14,701 yenye thamani ya Dola za Marekani 60,535,001.58 mpaka tani 44,103 yenye thamani ya Dola 286,669,500 ifikapo mwaka 2028/2029.

Hivyo, kwa unyenyekevu mkubwa napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia na kuzindua utekelezaji wa mpango huu.



**Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb)**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**

## SHUKRANI




Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anatoa shukrani kwa Menejimenti na Watumishi wa Wizara, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Vyama vya wafugaji kwa mchango na mawazo yaliyowezesha kutengeneza mpango huu.

Aidha, shukrani za dhati ziende kwa Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Taasisi ya Afya ya Ifakara (IHI), The Global Animal Health Tanzania (GAHT), Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwaafrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU-IBAR) kwa mchango wao kupitia miradi mbalimbali iliyosaidia katika kuandaa na utekelezaji wa mpango huu.

Vilevile, shukurani ziende kwa vyama vya kitaaluma ikiwepo Chama cha Madaktari wa Wanyama (TVA), Chama cha Madaktari wa Mifugo Wasaidizi (TAVEPA), watoa huduma za mifugo katika Sekta binafsi na wataalamu mbalimbali waliohusika katika uandishi na uhariri wa Mpango huu.

Mpango huu, ni mwanzo wa mafanikio makubwa kuelekea katika mapinduzi ya Sekta ya Mifugo kuwa ya kisasa, kibiashara na endelevu, hivyo kuongeza tija katika uzalishaji mifugo na mazao ya mifugo na kufungua Masoko ya Kikanda na Kimataifa.



Prof. Riziki S. Shemdoe
**KATIBU MKUU**

## YALIYOMO

DIBAJI........................................................................................................................ i

SHUKRANI..................................................................................................................... ii

YALIYOMO ................................................................................................................. iii

VIFUPISHO.................................................................................................................... v

1.0 UTANGULIZI............................................................................................................ 1

1.1 Hali Halisi ya Utambuzi na Uchanjaji Nchini........................................................................ 3

1.1.1 Utambuzi .................................................................................................................. 3

1.1.2 Uchanjaji..................................................................................................................... 4

1.2. Umuhimu wa kuchanja mifugo kwa uchumi na afya ya jamii ............................................... 5

2.0 MALENGO YA MPANGO ................................................................................................ 7

2.1 Lengo kuu.................................................................................................................... 7

2.2 Malengo Mahususi ......................................................................................................... 8

3.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUFANYIKA............................................................................... 8

3.1 Kutokomeza ugonjwa wa CBPP na PPR ifikapo 2029 ............................................................ 8

3.2 Kuongeza kiwango cha uchanjaji dhidi ya magonjwa ya kipaumbele ...................................... 9

3.3 Uchanjaji kuku wa asili Dhidi ya Magonjwa ya Mdondo, Mafua na Ndui ............................. 10

3.3.1 Matokeo ya Uchanjaji wa kuku Dhidi ya Magonjwa ya Mdondo Mafua na Ndui ............... 11

3.4 Ujenzi na usanifu wa mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa afya za Mifugo ........... 11

3.4.1 Matokeo ya Ujenzi na usanifu wa mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa afya za Mifugo............................................................................................................................. 11

3.5 Utambuzi wa Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo ........................................................................ 12

3.6 Uimarishaji wa mnyororo baridi wa kutunza chanjo .......................................................... 12

3.7 Uanzishwaji wa maeneo 25 huru ya magonjwa ya mifugo .................................................. 13

3.8 Utengenezaji wa ajira kwa Vijana wenye taaluma ya mifugo wasio kuwa kwenye mfumo rasmi wa ajira za Serikali.................................................................................................... 14

3.9 Ushirikishaji wadau ikiwemo Sekta binafsi kuandaa na kupitisha Mpango kazi wa chanjo utakaoendana na mazingira ya Kitanzania ................................................................... 15

3.10 Uhamasishaji kwa wadau wa mifugo kuhusu umuhimu wa chanjo .................................... 15

3.11 Ufuatiliaji na tathmini (M&E) ya mpango wa chanjo na utambuzi kitaifa .......................... 16

4.0 ENEO LA MKAKATI ..................................................................................................... 17

7. MATOKEO TARAJIWA YA MPANGO WA CHANJO NA UTAMBUZI WA MIFUGO.... 23

7.1 Kupata uthibitisho wa Shirika la Afya ya Wanyama Duniani ........................................ 24
7.2 Kuongezeka kwa biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi ......................................... 24
7.3 Kuongezeka biashara ya mazao ya mifugo ndani na nje ya nchi .............................. 25
7.4 Kulinda afya ya jamii......................................................................................................25
7.5 Kupunguza matumizi ya dawa za matibabu kwa mifugo............................................ 25
7.6 Kuongeza ajira ............................................................................................................. 26
8.0 WANUFAIKA WA ZOEZI LA CHANJO ............................................................................ 26
9.0 UZINDUZI WA KAMPENI YA CHANJO NA UTAMBUZI WA MIFUGO KITAIFA ....... 26
10.0 UENDELEVU WA SHUGHULI ZA UTAMBUZI NA UCHANJAJI ............................... 27
11.0 MPANGOKAZI NA GHARAMA ZA UTEKELEZAJI WA UTAMBUZI NA UCHANJAJI27
Kiambatisho 1. Gharama za Utambuzi na Utoaji chanjo kwa magonjwa ya kipaumbele kugharamiwa na Serikali kuanzia 2024/2025 - 2028/2029......................... 28

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **AU-IBAR** | Africa Union Inter-African Bureau for Animal Resources (Shirika la Umoja wa Afrika la Raslimali za Wanyama) |
| **BQ** | Black Quarter (Chambavu) |
| **CBPP** | Contagious Bovine Pleuropneumonia (Homa ya Mapafu ya Ng'ombe) |
| **CCPP** | Contagious Caprine Pleuropneumonia (Homa ya Mapafu ya Mbuzi ) |
| **DVS** | Director of Veterinary Services (Mkurugenzi Huduma za Mifugo) |
| **EAC** | East Africa Community (Jumuiya ya Afrika ya Mashariki) |
| **ECF** | East Cost Fever (Ndigana Kali) |
| **FAO** | Food and Agriculture Organisation (Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa) |
| **FMD** | Foot and Mouth Disease (Ugonjwa wa Miguu na Midomo) |
| **FOB** | Free on Board |
| **GAHT** | *Global Animal Health Tanzania* |
| **IFAD** | International Fund for Agricultural Development (Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo) |
| **IHI** | Ifakara Health Institute (Taasisi ya Afya ya Ifakara) |
| **LGA** | Local Government Authority |
| **LSD** | Lumpy Skin Disease (Mapele Ngozi) |
| **M&E** | Monitoring and Evaluation |
| **MSM** | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| **ND** | Newcasttle Disease (Mdondo/Kideri) |
| **NOVABI** | Nobel Vaccines and Biologicals |
| **OR-TAMISEMI** | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **PPR** | Peste des Petits Ruminant (Sotoka ya Mbuzi na Kondoo) |
| **RVF** | Riftvalley Fever (Homa ya Bonde la Ufa) |
| **SADC** | Southern Africa Development Community (Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwaAfrika) |
| **TAVEPA** | Tanzania Paraprofessional Association (Chama cha Madaktari wa |

| | |
|---|---|
| | Mifugo Wasaidizi Tanzania) |
| **TEHAMA** | Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TVA** | Tanzania Veterinary Association (Chama cha Madaktari wa Mifugo Tanzania) |
| **TVI** | Tanzania Vaccine Insititute (Taasisi ya Uzalishaji Chanjo Tanzania) |
| **TVLA** | Tanzania Veterinary Laboratory Agency (Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania) |
| **UVIDA** | Usugu wa Vimelea dhidi ya Dawa |
| **WOAH** | World Organisation for Animal Health (Shirika la Afya ya Wanyama Duniani) |
| **WTO** | World Trade Organization (Shirika la Biashara Duniani) |
| **ZVC** | Zonal Veterinary Center (Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo vya Kanda) |
| **ZVC** | United State Dollar |

## 1.0 UTANGULIZI

Tanzania ina takriban ng'ombe mil. 37.9, mbuzi 27.6, Kondoo 9.4, kuku 103.1 na nguruwe 3.9. Sekta hii huajiri asilimia 50 ya wakazi wake, sawa na kaya milioni 4.6 ambazo mapato yake hutegemea mifugo. Sekta ya mifugo ina mchango mkubwa katika kujenga uchumi imara wa taifa kwa kuongeza uhakika wa chakula cha kaya, kipato, nguvu kazi kupitia wanyama, mbolea na kuingiza fedha za kigeni kutokana na mauzo ya mifugo hai na mazao yake nje ya nchi. Sekta hii huchangia asilimia 6.2 kwenye pato ghafi la Taifa. Moja ya sababu za mchango mdogo kwenye pato ni pamoja na uwepo wa magonjwa yanayopunguza tija ya uzalishaji, kupunguza ubora wa mazao ya mifugo, husababisha vifo na kuathiri biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi. Kwa kutambua umuhimu wa kudhibiti magonjwa ya mifugo, Serikali iliainisha magonjwa 13 ya kipaumbele ambayo ni Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP), Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP), Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD), Mapele Ngozi (LSD), Ugonjwa wa kutupa Mimba (Brucellosis), Kimeta (Anthrax), Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR), Ndigana Kali (ECF), Mdondo (ND), Marek, Gumboro, Kichaa cha Mbwa (Rabies) na Homa ya Bonde la Ufa (RVF).

Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeandaa Mpango wa Chanjo na Utambuzi wa Mifugo kwa miaka mitano 2024 – 2029, dhidi ya magonjwa ya kipaumbele na inatarajia kutekeleza Mpango huo kwa kuanza na uzinduzi wa Kampeni ya Chanjo ya Mifugo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa. Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi 216,140,097,000 kwa kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa mpango huu. Kwa mwaka 2024/2025 Wizara imetenga jumla ya shilingi 69,262,059,000 ili kutekeleza Kampeni hiyo muhimu kitaifa ambayo imelenga kudhibiti na kutokomeza magonjwa ambayo ni kikwazo dhidi ya biashara ya mifugo na mazao yake kimataifa. Kupitia uchanjaji, mifugo itaongeza tija katika uzalishaji wa mifugo, kuongeza kiwango cha uuzaji wa

mazao ya mifugo nje ya nchi, kukuza pato la fedha za kigeni nchini. Aidha, Mpango huu wa uchanjaji wa mifugo utaongeza hamasa na muamko wa matumizi ya chanjo miongoni mwa wafugaji kutokana na kuwepo kwa kipengele cha uhamasishaji na ruzuku ya Serikali, hivyo kufikia adhma ambayo Tanzania imejiwekea ya kuwa eneo huru dhidi ya magonjwa ya mifugo.

Aidha, umuhimu wa utekelezaji wa Kampeni ya chanjo Kitaifa umesisitizwa katika hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati akifunga maonesho ya Nanene kitaifa kwa mwaka 2024 na wakati akiongea na Maafisa Ugani wa Kilimo Ikulu, Chamwino - Dodoma tarehe 10, Agosti 2024 ambapo aliridhia kufanyika kwa mpango wa Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa; na kwamba ufanyike kwa weledi kwa manufaa ya wafugaji na nchi kwa ujumla.

Juhudi zimekuwa zikifanyika kuhakikisha chanjo dhidi ya magonjwa ya kipaumbele zinapatikana na uchanjaji kufanyika kwa ufanisi. Juhudi hizi ni kupitia wazalishaji wa chanjo, waagizaji wa chanjo nje ya nchi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, watoa huduma wa Sekta binafasi na wafugaji. Ili kurahisisha upatikanaji wa chanjo, Serikali imevutia uwekezaji katika uzalishaji wa chanjo, ambapo hadi kufikia mwaka 2025 kuna viwanda vitatu vya kuzalisha chanjo nchini. Viwanda hivyo ni Tanzania Vaccine Institute (TVI) kinachozalisha aina saba za chanjo, Kiwanda cha Hester Bioscience Africa Limited kinachozalisha chanjo aina 37 na Kiwanda cha Nobel Vaccines and Biologicals Company Limited (NOVABI) Kinachozalisha chanjo ya kuku.

Chanjo ni njia rahisi, salama, na madhubuti ya kukinga wanyama dhidi ya magonjwa mbalimbali yanayosababishwa na vimelea. Kwa kuzingatia umuhimu wa chanjo, Wizara iliandaa Kanuni ya Chanjo na Uchanjaji – The Animal Diseases (Vaccines and Vaccination) Regulations 2020 chini ya Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya Mwaka 2003. Kanuni hii inamlazimisha kila mfugaji kuchanja mifugo yake dhidi ya magonjwa ya kipaumbele kulingana na Kalenda ya chanjo iliyotolewa na Wizara. Aidha, Wizara ilitengeneza Mwongozo wa Utoaji wa Chanjo dhidi ya Magonjwa ya Mifugo kwa mfumo wa ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi wa Mwaka 2021.

## 1.1 Hali Halisi ya Utambuzi na Uchanjaji Nchini

### 1.1.1 Utambuzi

Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo unafaida nyingi ikiwa ni pamoja na kuwezesha biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi; Kuwezesha upatikanaji wa bima na mikopo; Kudhibiti magonjwa ya milipuko; Kukabiliana na wizi na kurahisisha upatikanaji wa mifugo iliyopotea; na Kuwa na hakikisho la usalama wa chakula.

Katika kuhakikisha ufanisi wa zoezi la Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo linafanikiwa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatekeleza Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Sura 184 ya Mwaka 2010 na Kanuni zake za Mwaka 2011 na miongozo mbambali. Katika mwaka 2021/2022 Serikali ilitambua jumla ya mifugo 5,316,738 (ng’ombe 4,484,354; punda 66,863; mbuzi 513,729; kondoo 251,792) sawa na asilimia 11.6 ya lengo la kutambua jumla ya mifugo 45,920,000 kwa kutumia hereni za kielektroniki. Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imekusudia kutambua jumla ya mifugo 36,323,300 (ng’ombe 19,099,100; mbuzi na kondoo 17,224,200).

### 1.1.2 Uchanjaji

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikishirikiana na wadau katika sekta ya mifugo inafanya jitihada za kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mifugo. Wizara pia iliandaa orodha ya magonjwa ya kipaumbele ambayo mengi hutokea kwa njia ya mlipuko na hudhibitiwa kwa njia ya chanjo na kuogesha dawa za kuua kupe na wadudu wengine. Magonjwa kwa mifugo ni kikwazo kwa ufugaji, wafugaji, afya ya jamii na biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ya mifugo inatekeleza mikakati mbalimbali ya kudhibiti magonjwa ya mifugo. Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa katika kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe na kupe wenyewe kupitia ujenzi wa majosho na dawa zenye ruzuku kupitia kampeni kabambe ya uogeshaji. Sambamba na hilo, ili kuendeleza mapambano dhidi ya magonjwa ya mifugo kwa njia ya chanjo, kwa mwaka 2023/2024 jumla ya dozi za chanjo 695,978,188 zimetumika ambapo kati ya hizo, dozi 520,153,000 zimeingizwa kutoka nje ya nchi na dozi 175,825,188 zimezalishwa ndani ya nchi kwa ajili ya kuchanja magonjwa 13 ya kipaumbele. Kati ya dozi hizo zilizozalishwa nchini, dozi 62,173850 zimetengenezwa na Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) na dozi 113,651,338 zimezalishwa na Sekta Binafsi.

Wizara, kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine imeendelea kudhibiti magonjwa ya mifugo kupitia uchanjaji, uogeshaji mifugo na utoaji elimu kuhusu udhibiti wa magonjwa ya mifugo. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya dozi 616,070,986 zimetumika kuchanja mifugo dhidi ya magonjwa 13 ya kipaumbele ambayo ni: Kimeta kwa Ng’ombe, Mbuzi na Kondoo dozi 1,521,495; Kichaa cha mbwa na paka dozi 991,346; Homa ya Mapafu ya Ng’ombe dozi 5,734,881; Ugonjwa wa Miguu na Midomo kwa Ng’ombe dozi 2,523,786; Sotoka ya Mbuzi na Kondoo dozi 3,780,210; Mdondo dozi 296,479,000; Gumboro dozi 220,829,000; Ndigana Kali dozi 95,681 na Mahepe (*Marecks*) dozi 61,243,770; Chambavu (BQ) dozi 883,100; Ugonjwa wa Kutupa

Mimba dozi 53,975; Mapele ya Ngozi dozi 106,011 na Ndui ya Kuku dozi 21,828,713.

Uchanjaji huu usioratibiwa Kitaifa uliwezesha kukinga mifugo dhidi ya ugonjwa kwa kufikia asilimia 22 tu ambacho ni kiwango cha chini katika kudhibiti magonjwa. Mpango huu wa miaka mitano unaoratibiwa na Serikali umelenga kutokomeza magonjwa ya mifugo kwa kuchanja mifugo kutoka asilimia 22 ya sasa hadi kufikia zaidi ya asilimia 70 ya mifugo inayolengwa kuchanjwa ugonjwa husika kwa miaka mitano mfululizo. Baadhi ya changamoto zinazochangia uchanjaji kutokufanyika kwa ufanisi ni pamoja na: upatikanaji na usambazaji wa chanjo kwa wakati; gharama kubwa za baadhi ya chanjo; kutokuwepo kwa mfumo baridi wa uhakika, uhaba wa wataalamu wa mifugo katika Sekta ya umma, uhaba wa fedha, ushirikiano hafifu kati ya Sekta ya umma na binafsi na uelewa mdogo kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa chanjo.

## 1.2. Umuhimu wa kuchanja mifugo kwa uchumi na afya ya jamii

Pamoja na utajiri wa rasilimali za mifugo uliopo nchini, magonjwa yameendelea kuwa kikwazo cha uzalishaji wa mifugo, biashara ya mifugo na mazao ya mifugo. Changamoto nyingine ni uwepo wa magonjwa yanayotoka kwa wanyama na kuathiri binadamu na matumizi ya dawa za mifugo yasiyokuwa ya lazima ambayo yamekuwa chanzo kikuu cha Usugu wa Vimelea dhidi ya Dawa (UVIDA). Baada ya Awamu ya Sita kuifungua nchi kwa diplomasia ya uchumi, nchi nyingi zipo tayari kufanya biashara ya Mifugo na mazao yake na Tanzania. Hata hivyo, kutokana na changamoto ya magonjwa na kutokutekelezwa kwa viwango kwa mpango wa udhibiti wa magonjwa ya wanyama, nchi imeshindwa kuuza mifugo na mazao ya mifugo kiasi cha tani 882,182.8 zenye thamani ya USD 52,281,096,800 ambayo sawa na shilingi 139,851,933,940,000 kwa mwaka. Vilevile, magonjwa yameendelea kusababisha vifo kwa mifugo na kusababisha hasara.

Kuchanja mifugo kwa njia ya kampeni inayosimamiwa na Seriali ni njia rahisi ya kutokomeza magonjwa kwa vile inahakikisha mifugo zaidi ya 70% kuchanjwa kwa wakati mmoja sawa na ushauri wa kitaalamu wa Shirika la Afya ya Wanyama Duniani. Udhibiti wa magonjwa yenye umuhimu kibiashara una tija kubwa kwa Serikali na katika mnyororo wa thamani wa mifugo. Hivyo, ili kufikia malengo ya kutokomeza magonjwa na kuwa na maeneo huru kwa ajili ya kukuza biashara ya mifugo na mazao mifugo kikanda na kimataifa, uchanjaji wa mifugo kwa njia ya kampeni ugharamiwe na kusimamiwa na Serikali.

Aidha, mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe unapotokea husababisha hasara ya takribani Shilingi 123,991,259,000 kutokana na matibabu na vifo kwa mwaka. Gharama hii ingeweza kupungua kwa kuchanja ng'ombe kwa shilingi 59,825,590,000 kwa mwaka. Aidha, gharama inayotokana na ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Mbuzi kwa mwaka ni Shilingi 123,248,320,000 kwa mwaka ambapo iwapo uchanjaji ungefanyika kwa mwaka ungetumia Shilingi 59,307,660,000. Vilevile, jumla ya Shilingi 79,866,000,000 hutumika kama gharama ya kutibu na hasara ya vifo vya mbuzi na kondoo kutokana na ugonjwa wa Sotoka ya mbuzi na kondoo ukilinganisha na shilingi 15,925,340,000 zitakazoweza kutumika kwenye chanjo.

Kwa upande wa afya ya jamii, zaidi ya asilimia 60 ya magonjwa ya binadamu huambukiza kutoka kwa wanyama (zoonosis) na yanasababisha madhara makubwa ikiwemo vifo. Kwa wastani mbwa, 2,030 huugua kichaa na kung'ata watu takribani 3,387 na kati ya hawa, 1,500 huugua kichaa cha mbwa na kufariki kila mwaka. Gharama ya chanjo na matibabu kwa binadamu aliyeng'atwa na mbwa mwenye kichaa ni takribani shilingi 300,000 na Serikali inatumia hadi shilingi 1,016,100,000 kutibu wahanga waliong'atwa na mbwa wenye kichaa kwa mwaka. Aidha, gharama ya kati ya Shilingi 26,090,000 na 40,150,000 tu ingetumika kuchanja mbwa 2,030 wanaopata kichaa cha mbwa kwa mwaka.

Iwapo magonjwa haya yatadhibitiwa manufaa yatakayopatikana ni pamoja na: kuongezeka kwa biashara ya mifugo nje ya nchi. Ikiwemo mbuzi na kondoo kutoka 20,478 wenye thamani (FOB) ya Dola za Marekani 787,615.4 wa sasa hadi kufikia 300,000 wenye thamani ya Dola 11,538,461.5 kwa mwaka 2029; na ng'ombe kutoka 9,294 wenye thamani ya Dola za Marekani 3,574,615.4 mpaka kufikia 50,000 wenye thamani ya Dola 19,230,769.2.

Pia, mauzo ya nyama nje ya nchi yataongezeka kutoka tani 14,701 yenye thamani ya Dola za Marekani 60,535,001.58 inayouzwa kwa sasa mpaka takribani tani 44,103 yenye thamani ya Dola 286,669,500. Aidha, maziwa kilo 287,549.8 yenye thamani (FOB) ya Dola za Marekani 403,567.7 zinazouzwa nje ya nchi kwa sasa mpaka kilo 950,000 yenye thamani (FOB) ya Dola 1,425,000 ifikapo mwaka 2028.

Aidha, matumizi ya dawa za antibiotiki kwa mifugo ni zaidi ya kilo milioni mbili kwa mwaka na kusababisha uwepo wa masalia ya dawa kwa asilimia 70 kwenye nyama ya kuku wa broila, asilimia 36 nyama ya ng'ombe na asilimia 36 ya maziwa. Hivyo, chanjo itapunguza matumizi ya dawa kwa mifugo kwa zaidi ya asilimia 40 ifikapo 2029 na kuweza kupungua kwa usugu wa vimelea dhidi ya dawa (UVIDA) na kulinda jamii kutokana na madhara ya masalia ya dawa kwenye mazao ya mifugo. Utekelezaji wa Mpango huu utatoa ajira kwa wataalamu wa afya ya mifugo 7,500 ambao watahusika katika utoaji wa chanjo katika maeneo mbalimbali nchini kwa muda wote wa zoezi la chanjo.

## 2.0 MALENGO YA MPANGO

### 2.1 Lengo kuu

Kuimarisha Sekta ya mifugo ili kuiwezesha kuwa na tija, kuchangia uchumi wa viwanda, kuimarisha biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi na kunufaisha wafugaji na wananchi kwa ujumla.

## 2.2 Malengo Mahususi

(i) Kuongeza kiwango cha uchanjaji dhidi ya magonjwa ya kipaumbele kutoka asilimia 22 mpaka asilimia 70 Ili kupunguza vifo, kuongeza uzalishaji na kuondoa vikwazo katika biashara ya kimataifa ifikapo 2029;

(ii) Kujenga na kusanifu mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa afya za Mifugo;

(iii) Kuimarisha mnyororo baridi (*cold chain*) wa kutunza chanjo katika maeneo huru ya magonjwa kwa asilimia 100 ifikapo 2029;

(iv) Kuwa na maeneo huru ya magonjwa katika mashamba 20 ya kuku wazazi, mashamba 30 ya ngo'mbe wa maziwa, mashamba 5 ya ng'ombe wa nyama na Mashamba 3 ya mbuzi na kondoo;

(v) Kutengeneza ajira za muda kwa vijana takribani 7,500 wenye taaluma ya mifugo kutoka kutoka nje ya mfumo wa ajira ya Serikali ifikapo 2029;

(vi) Kuhamasisha na kuongeza ufahamu kwa wadau wa mifugo kuhusu Umuhimu wa chanjo;

(vii) Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini (M&E) ya mpango wa chanjo na utambuzi kitaifa.

## 3.0 KAZI ZILIZOPANGWA KUFANYIKA

Katika kutekeleza malengo mahususi, shughuli mbalimbali zimepangwa kufanyika kama ifuatavyo:

## 3.1 Kutokomeza ugonjwa wa CBPP na PPR ifikapo 2029

Ili kutokomeza ugonjwa wa CBPP na PPR ifikapo 2029 Wizara kuwezesha uchanjaji kutoka asilimia 22 hadi 70 ili kupunguza magonjwa na vifo kwa wanyama na kuwezesha biashara ya mifugo na amzao yake ndani na nje ya nchi.

**Zoezi litahusisha kazi zifuatazo:**

(i) Kununua na kuwezesha upatikanaji wa chanjo za magonjwa ya homa ya mapafu ya ng'ombe, Homa ya Mapafu ya mbuzi na Sotoka ya mbuzi/Kondoo kulingana na ratiba ya uchanjaji;

(ii) Kununua vitendea kazi na vifaa vya uchanjaji kama vile sindano, maboksi ya kutunza chanjo, majokofu, pikipiki na vishikwambi kwaajili ya kumbukumbu;

(iii) Kufanya kampeni za uhamasishaji kabla na wakati wa uchanjaji;

(iv) Kufanya uchunguzi wa kimaabara kubainisha hali ya ugonjwa husika kabla na baada ya chanjo;

(v) Kuchanja mifugo;

(vi) Kufanya tathmini ya zoezi la uchanjaji baada ya chanjo kutolewa; na

(vii) Kuandaa andiko la kuomba Ithibati ya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani kuutambua mpango wa udhibiti na kisha mpango ithibati ya kuwa huru dhidi ya magonjwa ya PPR na CBPP.

### 3.1.1 Matokeo ya kutokomeza PPR na CBPP

Baada ya kutekeleza zoezi la kutokomeza ugonjwa wa CBPP na PPR kunaweza kuwa na ongezeko la uzalishaji wa mifugo, kuimarika kwa kipato cha wafugaji, kuwepo kwa ustawi wa usalama wa chakula, kushamiri kwa biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi na kupungua kwa matumizi ya fedha kwa matibabu ya mifugo na fidia kutokana na vifo vinavyotokana na magonjwa.

## 3.2 Kuongeza kiwango cha uchanjaji dhidi ya magonjwa ya kipaumbele

Ili kupunguza vifo, kuongeza uzalishaji na kuondoa vikwazo katika biashara ya kimataifa Wizara inakusudia kuongeza uchanjaji dhidi ya magonjwa ya Miguu na Midomi, Mapele ngozi , Homa ya mapafu ya mbuzi, Ndui ya mbuzi na kondoo, Kichaa cha mbwa na Homa ya kutupa mimba, kutoka asilimia 22 ya sasa mpaka asilimia 70.

**Zoezi litahusisha kazi zifuatazo:**

i) Kuwezesha upatikanaji wa chanjo za magonjwa ya Miguu na Midomo, Mapele ngozi, Homa ya mapafu ya mbuzi, Ndui ya mbuzi na kondoo, Kichaa cha mbwa, Homa ya kutupa mimba, Mdondo wa kuku, Mafua ya kuku na Ndui ya kuku;

ii) Kununua vitendea kazi na vifaa vya uchanjaji kama vile sindano, maboksi ya kutunza chanjo, majokofu, pikipiki na Vishikwambi kwaajili ya kumbukumbu;

iii) Kufanya kampeni za uhamasishaji kabla na wakati wa uchanjaji;
iv) Kufanya uchunguzi wa kimaabara kubainisha hali ya ugonjwa husika kabla na baada ya chanjo;
v) Kuchanja mifugo;
vi) Kufanya tathmini ya zoezi la uchanjaji baada ya chanjo kutolewa; na
vii) Kuandaa andiko la kuomba ithibati ya Shirika la afya ya Wanyama duniani kuutambua mpango wa udhibiti na kisha mpango ithibati ya kuwa huru dhidi ya magonjwa ya Ndui ya mbuzi na Kondoo na Homa ya Mapafu ya Mbuzi.

### 3.2.1 Matokeo ya kuongeza kiwango cha uchanjaji

Kwa kutekeleza zoezi la kuongeza kiwango cha uchanjaji dhidi ya magonjwa ya kipaumbele itapelekea kupungua kwa milipuko ya magonjwa, kuimarika kwa afya ya mifugo, kuongeza tija kwa wafugaji, kuimarisha usalama wa chakula nchini, kustawi kwa biashara ya mifugo, kupunguza matumizi ya dawa na gharama za matibabu, na kuimarisha uwezo wa mifumo ya afya ya mifugo.

## 3.3 Uchanjaji kuku wa asili Dhidi ya Magonjwa ya Mdondo, Mafua na Ndui

Ili kupunguza vifo na kuongeza uzalishaji, kuimarisha lishe ya jamii na kipato kwa kaya katika kuwawezesha wanawake na vijana, Wizara inakusudia kuchanja kuku dhidi ya magonjwa ya Mdondo, Mafua na Ndui ya kuku kwa zaidi ya asilimia 70.

**Ili kutekeleza jukumu hili, Wizara inakusudia kufanya kazi zifuatazo:**

i) Kuwezesha upatikanaji wa chanjo za magonjwa ya Mdondo, Mafua, na Ndui ya kuku;
ii) Kufanya kampeni za uhamasishaji kabla na wakati wa uchanjaji;
iii) Kufanya uchunguzi wa kimaabara kubainisha hali ya ugonjwa husika kabla na baada ya chanjo;
iv) Kuchanja Kuku; na
v) Kufanya tathmini ya zoezi la uchanjaji baada ya chanjo kutolewa.

### 3.3.1 Matokeo ya Uchanjaji wa kuku Dhidi ya Magonjwa ya Mdondo Mafua na Ndui

Uchanjaji wa kuku wa asili itasaidia kupunguza vifo vya kuku, kuimarika kwa afya ya kuku wa asili, kuongezeka kwa kipato cha kaya, kupungua kwa matumizi ya dawa za tiba kwa magonjwa ya kuku, kuhamasisha ufugaji endelevu wa kuku wa asili, kuku wa asili kuchangia zaidi usalama wa chakula, na kupunguza kuenea kwa magonjwa ya kuku katika jamii.

## 3.4 Ujenzi na usanifu wa mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa afya za Mifugo

Ili kutunza taarifa za wafugaji, mifugo na taarifa za afya ya mifugo, Wizara kupitia kitengo cha TEHAMA itaunda mfumo na kuandaa nyaraka za ujenzi wa mfumo (User guidlines, user matrix), kufanya majaribio (user acceptance test) kwa maafisa wa Wizara, Ofisi ya Waziri Mkuu, OR-TAMISEMI, Wizara ya Afya na Serikali Mtandao. Aidha, mafunzo ya usajili, utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo kwa waratibu wa zoezi la chanjo na maafisa TEHAMA wa Mamlaka za Serikali za mitaa (MSM). Wizara itahusika katika kutoa msaada wa kiufundi wakati wa zoezi la utambuzi na uchanjaji wa mifugo kwa maafisa kutoka MSM.

### 3.4.1 Matokeo ya Ujenzi na usanifu wa mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa afya za Mifugo

Katika ujenzi na usanifu wa mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa afya ya Mifugo kutasaidia kuimarisha ufuatiliaji wa afya ya mifugo, kutambua mifugo binafsi, kuhakikisha ulinzi wa afya ya umma, kusaidia katika utungaji wa sera na mipango ya maendeleo ya mifugo, kuimarisha biashara ya mifugo na bidhaa zake, kuwalinda wafugaji dhidi ya hasara, na kudhibiti wizi na uhamaji holela wa mifugo.

### 3.5 Utambuzi wa Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo

Ili kukidhi matakwa ya soko la mifugo na mazao ya mifugo kimataifa, Wizara imeandaa mfumo wa utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo. Mfumo utawezesha kutambua ng'ombe, mbuzi na Kondoo kwa asilimia 70. Aidha, mfumo huu utasaidia ufuatiliaji na uthibiti wa magonjwa, utunzaji wa kumbukumbu za uzalishaji, upatikanaji wa bima za mifugo na mikopo kwa wafugaji, pamoja na kusaidia katika udhibiti wa wizi wa mifugo.

**Ili kutekeleza jukumu hili kazi zifuatazo zitafanyika:**

i) Kununua vitendea kazi na vifaa vya utambuzi kama vile hereni za kielektroniki kwa Ng'ombe 19,099,100, mbuzi na kondoo 17,224,200 na vifaa vya kuvalisha hereni;

ii) Kununua vishikwambi 4,500 kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za utambuzi wa wafugaji na mifugo;

iii) Kufanya kampeni za uhamasishaji;

iv) Kufanya utambuzi wa mifugo; na

v) Kufanya tathmini ya zoezi la utambuzi.

#### 3.5.1 Matokeo ya Zoezi la Utambuzi wa mifugo

Utambuzi wa ng'ombe, mbuzi na kondoo ni hatua ya kimkakati kwa maendeleo ya sekta ya mifugo nchini. Utambuzi huo utasaidia kuimarisha usimamizi wa mifugo, kuongeza tija, kudhibiti magonjwa, na kufungua fursa za kiuchumi kwa wafugaji na taifa kwa ujumla.

### 3.6 Uimarishaji wa mnyororo baridi wa kutunza chanjo

Ili kuimarisha mnyororo baridi kwa ajili ya utunzaji wa chanjo kabla ya kupelekwa katika MSM, Wizara inakusudia kufanya kazi zifuatazo:

(i) Kununua na kusambaza majokofu na vibebea chanjo kwenye MSM 184;

(ii) Kununua na kujenga vyumba baridi (Cold rooms) katika vituo nane (8) vya kanda vya wizara; na
(iii) Kutoa mafunzo kwa wataalam wa afya ya mifugo juu ya uhifadhi wa chanjo na mnyororo baridi wa chanjo.

### 3.6.1 Matokeo ya Zoezi

Kuimarisha mnyororo baridi ni msingi muhimu wa mafanikio ya programu za chanjo kwa mifugo. Ni hatua ya kimkakati ambayo itapelekea uhifadhi bora wa chanjo kwa ubora unaotakiwa, kupunguza uharibifu na upotevu wa chanjo, kuboresha huduma za afya ya mifugo, na kudhibiti milipuko ya magonjwa ya mifugo kwa ufanisi zaidi.

## 3.7 Uanzishwaji wa maeneo 55 huru ya magonjwa ya mifugo

Uanzishwaji wa maeneo huru 55 yenye udhibiti mkubwa wa magonjwa ya mifugo ili kuimarisha biashara ya mifugo na mazao ya mifugo, Serikali inakusudia kuanzisha maeneo huru ya magonjwa katika mashamba 20 ya kuku wazazi, mashamba 15 ya ng'ombe wa maziwa, mashamba 15 ya ng'ombe wa nyama na mashamba 5 ya mbuzi na kondoo baada ya udhibiti wa magonjwa kwa njia ya chanjo na kutambua mifugo. Mifugo na mazao ya mifugo kutoka katika maeneo haya yatakuwa mahususi kwa biashara ya kimataifa.

**Katika kutekeleza jukumu hili kazi zifuatazo zinakusudiwa kufanyika: -**

i) Kuainisha mashamba ambayo yana kidhi vigezo vya kuwa maeneo huru ya magonjwa (Animal disease free compartment)
ii) Kufanya ufuatiliaji wa magonjwa ya Mifugo yote yaliyo ainishwa kama maeneo huru ya magonjwa (Disease surveillance and monitoring)
iii) Kukusanya sampuli nakufanyia uchunguzi kwenye maabara zenye ithibati ya nchi za Umoja wa Ulaya na Amerika.
iv) Kuandaa na kutoa vyeti vya kutambua na kuthibitisha mashamba ambayo yamekidhi vigezo vya kuwa eneo huru la magonjwa ya mifugo
v) Kuhuisha taarifa za maeneo huru ya magonjwa katika mfumo wa utambuzi.

### 3.7.1 Matokeo ya Zoezi

Matokeo yanayotarajiwa endapo Tanzania itaanzisha maeneo 55 huru dhidi ya magonjwa ya mifugo (disease free compartments) ni pamoja na kulinda afya ya mifugo, kuinua uchumi wa wafugaji, na kufungua fursa za kibiashara ndani na nje ya Tanzania.

## 3.8 Utengenezaji wa ajira kwa Vijana wenye taaluma ya mifugo wasio kuwa kwenye mfumo rasmi wa ajira za serikali

Ili kutekeleza jukumu hili Wizara inakusudia kutoa ajira kwa Vijana takribani 7,500 wenye taaluma ya mifugo wasio kuwa katika ajira rasmi ya Serikali.

Ili kutekeleza kazi hii, Wizara inakusudia kufanya yafuatayo:

(i) Kuhuisha orodha ya wataalamu wa afya ya mifugo walioko kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, taasis za Serikali zinazojitegemea na Sekta binafsi;

(ii) Kutangaza na kuandikisha wataalamu wa afya ya mifugo wasio katika mfumo rasmi wa ajira kushiriki katika zoezi la uchanjaji;

(iii) Kutoa mafunzo tarajali ya chanjo na uchanjaji wa mifugo kwa wataalam wa afya ya mifugo waliojiandikisha;

(iv) Kuwapangia vituo wataalamu wa afya ya mifugo waliojiandikisha na kuwasambaza na kuwasimamia kwenye maeneo mbalimbali ya nchi kwa ajili ya kuendesha zoezi la uchanjaji.

### 3.8.1 Matokeo ya Zoezi

Kutoa fursa za ajira kwa vijana wenye taaluma ya mifugo ni hatua muhimu kwa kuwa itapunguza ukosefu wa ajira kwa vijana, kuimarika kwa huduma ya afya ya mifugo katika maeneo ya vijijini na maeneo ya pembezoni, kuwezesha upatikanaji wa huduma kwa haraka na kwa gharama nafuu kwa wafugaji,

kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo, kujenga mazingira ya kujitegemea na ujasiriamali kwa vijana, kuchangia katika utekelezaji wa mipango ya taifa ya chanjo na kudhibiti magonjwa, na kuchochea ubunifu katika sekta ya mifugo.

## 3.9 Ushirikishaji wadau ikiwemo Sekta binafsi kuandaa na kupitisha Mpango kazi wa chanjo utakaoendana na mazingira ya Kitanzania

**Zoezi hili litahusisha:**

(i) Kuandaa mpangokazi wa utekelezaji wa utoaji chanjo unaoshirikisha wadau;

(ii) Kuandaa mikutano miwili ya kutengeneza mpangokazi kwa kuwatumia wadau mbalimbali;

(iii) Kuandaa mkutano wa wadau kupitisha mpangokazi (*Validation meeting)*;

(iv) Kuchapisha, kusambaza na kutoa mafunzo kwa watekelezaji wa mpangokazi uliondaliwa; na

(v) Uzinduzi wa Mpangokazi wa uchanjaji na zoezi la uchanjaji.

### 3.9.1 Matokeo ya Zoezi

Kuhusisha wadau wakiwemo sekta binafsi, katika maandalizi na utekelezaji wa mpango wa chanjo ni muhimu kwa kuwa huongeza ufanisi, uendelevu na mafanikio ya juhudi za taifa katika kulinda afya ya mifugo na kuboresha maisha ya wafugaji.

## 3.10 Uhamasishaji kwa wadau wa mifugo kuhusu umuhimu wa chanjo

Kutakuwa na uhamasishaji kwa wadau wa mifugo kuhusu umuhimu wa chanjo na hatua muhimu ya kuhakikisha ushiriki wa jamii, afya bora ya mifugo na mafanikio ya mikakati ya taifa ya kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya mifugo.

**Zoezi hili Litahusisha Kazi Zifuatazo:**

(i) Kufanya zoezi la uhamasishaji kwa kutumia mikutano, majukwaa mbalimbali, vipindi vya redio, runinga, mabango, vipeperusihi na notisi za kuhamasisha ushiriki katika zoezi la chanjo;

(ii) Kutoa hamasa ya uchanjaji na faida za chanjo kwa kwa wafugaji.

(iii) Kufuatilia fursa ya biashara ya raslimali ya mifugo katika mataifa mbalimbali kwa kutangaza mpango huu unavyotekelezwa nchini kudhibiti magonjwa.

### 3.10.1 Matokeo ya Zoezi

Matokeo yanayoweza kupatikana endapo Tanzania itatekeleza kwa ufanisi mpango wa uhamasishaji kwa wadau wa mifugo kuhusu umuhimu wa chanjo. Vilevile, kuongezeka kwa uelewa kuhusu faida za chanjo kwa mifugo kuongezeka kwa ushiriki wa wafugaji kwenye kampeni za chanjo, kupungua kwa milipuko ya magonjwa ya mifugo, kuboresha uzalishaji wa mifugo na kipato cha wafugaji, kuongeza mahusiano na ushirikiano kati ya wafugaji na wataalamu wa mifugo, kuwezesha upatikanaji wa takwimu sahihi za mifugo na chanjo, na kupunguza matumizi ya dawa zisizo rasmi au zisizo sahihi.

## 3.11 Ufuatiliaji na tathmini (M&E) ya mpango wa chanjo na utambuzi kitaifa

Ufuatiliaji na tathmini ya Mpango wa Chanjo na Utambuzi ni muhimu katika kusaidia kuhakikisha uwazi, ufanisi na uwajibikaji katika utekelezaji wa mpango wa kitaifa wa chanjo na utambuzi wa mifugo. Pia utatoa msingi wa kufanya maamuzi yenye ushahidi (evidence-based policy making) kwa maendeleo ya sekta ya mifugo nchini Tanzania.

Zoezi hili litahusisha kazi zifuatazo:

(i) Kuwezesha wataalam kufanya ufuatiliaji wa zoezi la uchanjaji;

(ii) Kufanya vikao vya ufuatiliaji na kuchakata taarifa za jinsi ya zoezi linavyoendelea na uboreshaji wake; na

(iii) Kufanya mikutano ya tathimini ya zoezi la uchanjaji kabla ya kuanza zoezi, katikati ya zoezi (midterm review) na mwisho wa zoezi (end term review).

### 3.11.1 Matokeo ya Zoezi la Ufuatiliaji na Tathmini

Matokeo ya zoezi la ufuatiliaji na tathmini ya Mpango wa Chanjo na Utambuzi ni kusaidia kuhakikisha upatikanaji wa ripoti za mara kwa mara za maendeleo ya utekelezaji wa mpango, kuwa na mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa, kuwa na hifadhidata ya mifugo iliyotambuliwa na kuchanjwa, kuwa na viwango vya utendaji vilivyofuatiliwa kama vile asilimia ya mifugo waliopata chanjo kulingana na walengwa, idadi ya watoa huduma waliopatiwa mafunzo, idadi ya mifugo iliyosajiliwa na kutambuliwa pia kuwa na ripoti za tathmini ya athari za chanjo.

## 4.0 ENEO LA MKAKATI

Mpango wa utambuzi na uchanjaji utatekelezwa kwenye MSM 184 kwa kulenga magonjwa 12 ya kipaumbele. Katika awamu ya kwanza, utahusisha magonjwa ya Homa ya mapafu ya Ng'ombe, Sotoka ya Mbuzi na kondoo, Kideri/Mdondo wa kuku, Ndui ya kuku na Mafua ya kuku. Aidha, katika awamu zinazofuata magonjwa mengine yatakayo husika ni pamoja na Midomo na Miguu, Kichaa cha Mbwa, Ndui, Mapele Ngozi, Homa ya mapafu ya mbuzi.

**Jedwali 1:** Aina ya chanjo itakayotolewa, eneo, lengo na muda wa utekelezaji wa zoezi la chanjo awamu ya kwanza

| Na | Aina ya chanjo | Aina ya wanyama | Eneo | Lengo | Muda |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Homa ya Mapafu ya ng'ombe | Ng'ombe | MSM 184 | Kutokomeza ifikapo 2029 | Miaka 5 |
| 2 | Sotoka ya Mbuzi na Kondoo | Mbuzi na | MSM 184 | Kutokomeza ifikapo 2029 | Miaka 5 |

| Na | Aina ya chanjo | Aina ya wanyama | Eneo | Lengo | Muda |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kondoo | | | |
| 3 | Homa ya mapafu ya mbuzi | Mbuzi | MSM 184 | Kutokomeza | Miaka 5 |
| 4 | Ndui ya mbuzi na Kondoo | Mbuzi na Kondoo | MSM 184 | Kutokomeza | Miaka 5 |
| 5 | Ugonjwa wa miguu na midomo | Ng'ombe | Maeneo huru yamagonjwa | Kuwa na maeneo huru ya magonjwa kwa ajili ya biashara za nje | Miaka 5 |
| 6 | Kichaa cha Mbwa (Rabies) | Mbwa na Paka | MSM 184 | Kutokomeza ifikapo 2030 | Miaka 5 |
| 7 | Homa ya kutupa mimba (Brucellosis) | Ng'ombe wa Maziwa | Maeneo kunakotekelezwa Mradi wa IFAD | Kulinda afya ya Jamii | Miaka 5 |
| 8 | Ndigana kali (ECF) | Ng'ombe | Maeneo kunakotekelezwa mradi wa IFAD | Kupunguza maambukizi | Miaka 5 |
| 9 | Mapele Ngozi | Ngo'mbe | MSM 184 | Kutokomeza | Miaka 5 |
| 10 | Mdondo/Kideri | Kuku wa Asili | MSM184 | Kupunguza maabukizi | Miaka 5 |
| 11 | Ndui ya Kuku | Kuku wa Asili | MSM 184 | Kupunguza maabukizi | Miaka 5 |
| 12 | Mafua ya kuku | Kuku wa Asili | MSM 184 | Kupunguza maabukizi | Miaka 5 |

## 5.0 UTEKELEZAJI NA GHARAMA ZA MPANGO

Mpango wa utambuzi na uchanjaji unatarajia kugharimu jumla ya shilingi 216,140,097,000 kwa kipindi cha miaka (5) ambapo utoaji chanjo utafanyika kwa njia ya kampeni ili kutokomeza magonjwa ya Homa ya mapafu ya ng'ombe, Homa ya Mapafu ya mbuzi, Sotoka ya mbuzi na kondoo, Ndui ya mbuzi na kondoo, Mapele Ngozi na Ugonjwa wa Kichaa cha mbwa. Aidha, mpango

unalenga kudhibiti magonjwa mengine ili kuongeza tija katika ufugaji, kuongeza fursa za kibiashara na kulinda afya ya jamii.

Utengenezaji wa maeneo huru utagharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali na sekta binafsi. Mashamba ya Serikali na sekta binafsi yatakayo ainishwa na kufanyiwa tathmini yatapewa ithibati ya kutambuliwa kama maeneo huru ya magonjwa kwaajili ya biashara ya kimataifa. Kwenye maeneo hayo Serikali itaratibu upatinakaji wa chanjo na wenye mashamba watagharamia utoaji chanjo za FMD kwa kuzingatia ratiba.

Gharama za utekelezaji zinategemea kuwa kiasi cha Shs 216,140,097.000 kwa kipindi cha mitano (5) kuanzia 2024 mpaka 2029. Aidha, mchanganuo wa gharama hizi ni: mwaka 2024/2025 Shs 69,362,059,000, , mwaka 2026/2027 Shs 37,819,704,865, mwaka 2027/2028 Shs 35,509,304,865, mwaka 2027/2028 Shs 35,509,304,865 , na mwaka 2028/2029 Shs 35,589,323,405.

## 6.0 MAJUKUMU YA WADAU KATIKA UTEKELEZAJI WA MKAKATI

Mkakati huu utatekelezwa kwa ushirikiano na wadau mbalimbali ambao orodha na majukumu yao yameainishwa kwenye jedwali Na 2 hapa chini:

**Jedwali Na 2.** Wadau na majukumu yao katika kutekeleza mkakati huu

| Na | Mdau | Majukumu |
|---|---|---|
| 1 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi | (i) Kuandaa mpango wa utamuzi na chanjo na kuainisha maeneo ya kuchanja;<br>(ii) Kununua na kusambaza vifaa na chanjo pamoja na vitendea kazi;<br>(iii) Kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya mnyororo baridi wa chanjo;<br>(iv) Kuratibu, kuhamasisha na kuzindua zoezi la utambuzi na chanjo;<br>(v) Kuhuisha orodha na kuratibu watoa huduma za chanjo<br>(vi) Kusimamia utekelezaji wa ratiba ya chanjo;<br>(vii) Kushirikiana na wadau wakiwemo wadau wa maendeleo katika kuwezesha zoezi la chanjo. |
| 2 | Ofisi ya Rais TAMISEMI | (i) Kuunganisha Wizara na Tawala za Mikoa na MSM;<br>(ii) Kusimamia Sera, Sheria na kanuni zinazoongoza utoaji wa chanjo na utambuzi katika MSM;<br>(iii) Kuratibu kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa zoezi la chanjo;<br>(iv) Kufuatilia na kukagua utendaji wa MSM katika utoaji wa chanjo; |
| 3 | Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa | (i) Kuelekeza MSM katika maeneo yao katika utekelezaji wa Mpango kazi wa utambuzi na utoaji chanjo;<br>(ii) Kuhamamisha na kusimamia zoezi la utambuzi na utoaji chanjo katika MSM;<br>Kutunza kumbukumbu za watoa huduma za chanjo na uwezo wao. |
| 4 | Mamlaka za Serikali za Mitaa | (i) Kuhakikisha mifugo yote inatambuliwa na inapata chanjo kulingana na kalenda ya chanjo;<br>(ii) Kuratibu na kutekeleza zoezi la utambuzi na chanjo kwa kushirikisha watoa huduma binafsi na wataalamu walioko katika Halmashauri kulingana na kalenda ya chanjo;<br>(iii) Kuwashirikisha wahitimu wa udaktari wa mifugo, maafisa mifugo wasaidizi ambao hawajajiriwa walioko katika maeneo yao na kuwapokea wanaotoka maeneo kulingana na mahitaji;<br>(iv) Kuweka mikataba na wazabuni watakaotekeleza zoezi la usambazaji chanjo;<br>(v) Kushirikisha wafugaji na vyama vyao, Serikali za vijiji au mitaa katika utekelezaji wa zoezi la chanjo; |

| Na | Mdau | Majukumu |
|---|---|---|
| | | (vi) Kuhakikisha uwepo wa raslimali zitakazotumika kwenye zoezi la chanjo kama vile majokofu, usafiri, vibebea chanjo, sindano, mabomba ya chanjo kabla ya zoezi kuanza;<br>(vii) Kuandaa maeneo ya kuhifadhi chanjo na kuhakikisha mnyororo baridi unakuwepo wakati wote wa uchanjaji;<br>(viii) Kuweka utaratibu wa kutambua mifugo na wafugaji walioshiriki kwenye zoezi la chanjo;<br>(ix) Kudurufu na kusambaza daftari la kumbukumbu za chanjo kwa kila mfugaji;<br>(x) Kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kutathimini zoezi la chanjo kabla na baada ya chanjo; na Kutoa wasimamizi wa timu za uchanjaji. |
| 5 | Wazalishaji wa chanjo | (i) Kuwasilisha aina ya chanjo na kiwango wanachozalisha kwa WMU;<br>(ii) Kuzalisha chanjo zinazohitajika katika zoezi husika kwa wakati kwa kuzingatia ratiba;<br>(iii) Kushiriki katika uhamasishaji wa zoezi la chanjo kwa kushirikiana na wadau;<br>(iv) Kutoa maelekezo ya matumizi na utunzaji wa ubora wa chanjo kwa lugha inayoeleweka kwa watumiaji. |
| 6 | Waagizaji wa chanjo | (i) Kuagiza chanjo ambazo zinahitajika kwenye zoezi la chanjo ambazo uwezo wa kuzalishwa nchini haupo;<br>(ii) Kuhakikisha kuwa chanjo zinazoagizwa zimesajiliwa na Mamlaka ya Dawa Vifaa tiba na ama kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo. |
| 7 | Maabara za Veterinari na Vituo vya mifugo vya kanda | (i) Kutunza/kuhifadhi chanjo za Kanda husika kabla ya kupelekwa MSM;<br>(ii) Kuchukua na kupima sampli kabla na baada ya chanjo ili kudhibiti ubora wa chanjo na zoezi la chanjo;<br>(iii) Kusimamia zoezi la chanjo kwenye kanda husika;<br>(iv) Kutoa taarifa za zoezi la chanjo kwenye maeneo yao. |

| Na | Mdau | Majukumu |
|---|---|---|
| | | (vi) Kuhakikisha uwepo wa raslimali zitakazotumika kwenye zoezi la chanjo kama vile majokofu, usafiri, vibebea chanjo, sindano, mabomba ya chanjo kabla ya zoezi kuanza;<br>(vii) Kuandaa maeneo ya kuhifadhi chanjo na kuhakikisha mnyororo baridi unakuwepo wakati wote wa uchanjaji;<br>(viii) Kuweka utaratibu wa kutambua mifugo na wafugaji walioshiriki kwenye zoezi la chanjo;<br>(ix) Kudurufu na kusambaza daftari la kumbukumbu za chanjo kwa kila mfugaji;<br>(x) Kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kutathimini zoezi la chanjo kabla na baada ya chanjo; na Kutoa wasimamizi wa timu za uchanjaji. |
| 5 | Wazalishaji wa chanjo | (i) Kuwasilisha aina ya chanjo na kiwango wanachozalisha kwa WMU;<br>(ii) Kuzalisha chanjo zinazohitajika katika zoezi husika kwa wakati kwa kuzingatia ratiba;<br>(iii) Kushiriki katika uhamasishaji wa zoezi la chanjo kwa kushirikiana na wadau;<br>(iv) Kutoa maelekezo ya matumizi na utunzaji wa ubora wa chanjo kwa lugha inayoeleweka kwa watumiaji. |
| 6 | Waagizaji wa chanjo | (i) Kuagiza chanjo ambazo zinahitajika kwenye zoezi la chanjo ambazo uwezo wa kuzalishwa nchini haupo;<br>(ii) Kuhakikisha kuwa chanjo zinazoagizwa zimesajiliwa na Mamlaka ya Dawa Vifaa tiba na ama kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo. |
| 7 | Maabara za Veterinari na Vituo vya mifugo vya kanda | (i) Kutunza/kuhifadhi chanjo za Kanda husika kabla ya kupelekwa MSM;<br>(ii) Kuchukua na kupima sampli kabla na baada ya chanjo ili kudhibiti ubora wa chanjo na zoezi la chanjo;<br>(iii) Kusimamia zoezi la chanjo kwenye kanda husika;<br>(iv) Kutoa taarifa za zoezi la chanjo kwenye maeneo yao. |

| Na | Mdau | Majukumu |
|---|---|---|
| 8 | Makampuni ya utoaji wa chanjo na utambuzi ya Sekta Binafsi | (i) Kushiriki katika maandalizi ya awali ya Mpango kazi wa utambuzi na utoaji chanjo yatakayoshirikisha vikao na wadau;<br>(ii) Kuingia mikataba na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutoa huduma zinazohusiana na utoaji wa chanjo na utambuzi;<br>(iii) Kuhamasisha zoezi la utambuzi na chanjo kwa kushirikiana na vyama vya wafugaji;<br>(iv) Kutoa chanjo kwa kutumia chanjo zilizothibitishwa na kusajiliwa na TMDA au kuruhusiwa na DVS;<br>(v) Kuhakikisha kuwa chanjo zote zinakuwa kwenye mnyororo baridi;<br>(vi) Kutunza na kutuma kumbukumbu za chanjo kwa Daktari wa mifugo wa wilaya; na<br>(vii) Kujaza kumbukumbu kwenye daftari la kumbukumbu la mfugaji. |
| 9 | Wataalamu waliohitimu mafunzo ya afya ya mifugo walio nje ya mfumo wa ajira rasmi | (i) Kushiriki katika maandalizi ya awali ya utoaji wa chanjo na utambuzi yatakayoshirikisha vikao na wadau;<br>(ii) Kuhamasisha zoezi la utambuzi na chanjo kwa kushirikiana na vyama vya wafugaji;<br>(iii) Kutoa chanjo kwa kutumia chanjo zilizothibitishwa na kusajiliwa na TMDA au kuruhusiwa na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo;<br>(iv) Kuhakikisha kuwa chanjo zote zinakuwa kwenye mnyororo baridi;<br>(v) Kutunza na kutuma kumbukumbu za chanjo na utambuzi kwa Daktari wa mifugo wa wilaya; na<br>(vi) Kujaza kumbukumbu kwenye daftari la kumbukumbu la mfugaji. |
| 10 | Wafugaji | (i) Kushiriki katika kuandaa miundombinu ya kutolea huduma za chanjo na utambuzi;<br>(ii) Kushirikiana na viongozi wa vijiji/mitaa na vyama vya wafugaji kuhamasisha zoezi la utambuzi na chanjo kwa wafugaji wengine;<br>(iii) Kupeleka mifugo kwenye vituo vya chanjo na utambuzi kulingana na ratiba ya utoaji chanjo;<br>(iv) Kutoa taarifa kwa afisa mifugo au kiongozi mwingine wa Serikali kama kutakuwa na madhara yoyote yanayodhaniwa kuwa yametokana na chanjo au uchanjaji;<br>(v) Kuchangia gharama za chanjo kwa kulipia bei elekezi<br>(vi) Kutunza daftari la kumbukumbu za chanjo kwa lengo la |

| Na | Mdau | Majukumu |
|---|---|---|
| | | kufuatilia kiwango cha uchanjaji, ubora na watoa huduma pale linapohitajika. |
| 11 | Wadau wa Maendeleo | Kushirkiana na Wizara katika kufanikisha zoezi la utoaji wa chanjo kwa kutoa miongozo ya kitaalamu na rasilimali za kusaidia ulekelezaji wa mpango-kazi wa chanjo |
| 12 | Asasi za kiraia zinazojishughulisha na mifugo | (i) Kushirkina na Wizara katika kufanikisha zoezi la chanjo kwa kutoa miongozo ya kitaalamu na rasilimali za kutumika kwenye zoezi la chanjo;<br>(ii) Kuhamasisha zoezi la chanjo katika ngazi ya Jamii kwenye maeneo wanaypotoa huduma. |
| 13 | Waandishi wa habari | (i) Kushiriki katika kutangaza na kuhamasisha zoezi la utoaji wa chanjo;<br>(ii) Kushirikiana na kitengo cha habari cha Wizara kuutangazia umma kuhusiana na zoezi la chanjo na faida zake. |

## 7. MATOKEO TARAJIWA YA MPANGO WA CHANJO NA UTAMBUZI WA MIFUGO

Matokeo tarajiwa ya mpango wa chanjo na utambuzii utakaogharamiwa na Serikali, wadau katika sekta binafsi pamoja na wafugaji ni kutokomeza baadhi ya magonjwa, kupungua kwa magonjwa, kuongeza usalama wa chakula, kulinda afya ya jamii, kuongeza masoko ya ndani na nje ya nchi na kupunguza matumizi ya dawa za matibabu kwa mifugo. Aidha, ajira kwa vijana wataalamu wa mifugo walio nje ya mfumo rasmi wa ajira ya Serikali watanufaika na ajira za muda mfupi na hivyo kusaidia kuongezeka kwa huduma za ugani hata baada ya kumalizika kwa mpango huu.

Magonjwa yanayotarajiwa kutokomezwa nchini ni Homa ya Mapafu ya Ng’ombe, Homa ya Mapafu ya Mbuzi, Sotoka ya Mbuzi na Kondoo na Kichaa cha mbwa. Aidha, Ugonjwa wa Miguu na Midomo unatarajiwa kutokomezwa kwenye maeneo maalumu ya ranchi za Serikali na Binafsi (FMD free compartments). Vilevile, magonjwa yanayotarajiwa kupungua ni Ugonjwa wa Miguu na Midomo, Kimeta, Mapele ngozi, Kutupa mimba, Mdondo na Ndigana kali. Kudhibitiwa kwa magonjwa haya kutapelekea faida zifuatazo:

### 7.1 Kupata uthibitisho wa Shirika la Afya ya Wanyama Duniani

Tanzania kuwa ni nchi huru kwa magonjwa ya Homa ya mapafu ya ng’ombe, Homa ya Mapafu ya mbuzi, Sotoka ya mbuzi na kondoo, Ndui ya mbuzi na kondoo, na Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa;

### 7.2 Kuongezeka kwa biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi

(i) Ng’ombe 2,218,293 waliuzwa kwa mwaka 2022/2023 kwenye minada ndani ya nchi, kati ya hao ng’ombe 9,294 wenye thamani ya Dola za Marekani 3,574,615.4 pekee ndiyo waliuzwa nje ya nchi. Kiwango cha mauzo nje ya nchi kinaweza kuongezeka hadi kufikia 55,764 thamani ya Dola 21,447,692.3 ifikapo 2029,

(ii) Mbuzi na Kondoo 2, 121,187 waliuzwa kwa mwaka 2022/2023 kwenye minada ya ndani ya nchi kati ya hao mbuzi na kondoo 20,478 wenye thamani ya Dola za Marekani 787,615.4 ndio waliuzwa nje ya nchi. Kiwango cha mauzo nje ya nchi kinaweza kuongezeka hadi kufikia 307,170 wenye thamani ya Dola 11,814,230.7 ifikapo 2029;

(iii) Vifaranga wa kuku 83,845,967 walizalishwa mwaka 2022/2023 ndani ya nchi kati yao vifaranga 428,695 wenye thamani ya Dola za Marekani 274,804.5 tu ndio waliuzwa nje ya nchi. Kiwango cha mauzo nje ya nchi kinaweza kuongezeka hadi kufikia milioni 2 wenye thamani ya Dola 1,282,051.3 ifikapo 2029.

### 7.3 Kuongezeka biashara ya mazao ya mifugo ndani na nje ya nchi

(i) Nyama: Usafirishaji wa nyama nje ya nchi tani 14,701 kwa mwaka 2023/2024 zenye thamani ya Dola za Marekani 60,535,001.58. Kiwango hiki kinaweza kuongezeka hadi mara tatu ya kiwango cha juu cha sasa na kufikia tani 44,103 chenye thamani ya Dola 286,669,500 ifikapo mwaka 2029.

(ii) Maziwa: Uzalishaji wa maziwa nchini kwa mwaka 2023/2024 ni kilo bilioni 3.6 ambapo kilo 287,549.8 zenye thamani (FOB) ya Dola za Marekani 403,567.7 tu ndio ziliuzwa nje ya nchi. Kiwango hiki kinaweza kuongezeka hadi kufikia kilo 950,000 zenye thamani (FOB) ya Dola 1,425,000 ifikapo mwaka 2029

(iii) Mayai: Uzalishaji wa mayai nchini kwa mwaka 2023/2024 ni bilioni 5.5 ambapo mayai 1,643,720 tu yameuzwa nje ya nchi. Kiwango hiki kinaweza kuongezeka hadi kufikia mayai milioni 3 ifikapo 2029.

### 7.4 Kulinda afya ya jamii

Takribani asilimia 60 ya magonjwa ya milipuko yanatoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, uchanjaji wa mifugo utasaidia kutokomezwa kwa baadhi ya magonjwa ya mifugo na kupunguza maambukizi ya magonjwa ya Wanyama kwenda kwa binadamu.

### 7.5 Kupunguza matumizi ya dawa za matibabu kwa mifugo

Matumizi makubwa ya dawa katika sekta ya mifugo yanasababisha usugu wa vimelea dhidi ya dawa (UVIDA). UVIDA kwa sasa ni tatizo kubwa na linatishia ufanisi wa matibabu kwa binadamu na wanyama. Wafugaji hupendelea kutibu mifugo yao inapougua hata kwa magonjwa yanayoweza kukingwa kwa chanjo. Endapo magonjwa yatadhibitiwa kwa chanjo, matumizi ya dawa yatapungua kwa kiwango kikubwa na hivyo kuzuia usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa.

## 7.6 Kuongeza ajira

Utoaji chanjo kwa njia ya kampeni unatoa fursa ya ajira za moja kwa moja na ajira kwenye mnyororo wa thamani. Ajira za moja kwa moja zinahusisha wataalam wa afya ya mifugo 7,500 waliopo nje ya mfumo rasmi wa ajira katika kutoa huduma ya chanjo. Aidha, ajira zitaongezeka miongoni mwa wadau kwenye mnyororo wa thamani wa mifugo hususan wafanyabiashara wa chanjo, mifugo na mazao yake, viwanda vya kuzalisha chanjo na kuchakata mazao ya mifugo.

## 8.0 WANUFAIKA WA ZOEZI LA CHANJO

Utekelezaji wa mkakati huu utawanufaisha wadau mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Wataalamu wa afya ya wanyama zaidi ya 7,500 walioko nje ya mfumo rasmi wa ajira;
(ii) Wafugaji zaidi ya kaya 4,202,744;
(iii) Wafanyabiashara wa mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi;
(iv) Viwanda vitatu (3) vya kuzalisha chanjo;
(v) Viwanda 397 vya kuchakata mazao ya mifugo (nyama 24, maziwa 152, vyakula vya mifugo 221);
(vi) Wafanyabiashara 180 wa vifaa vya minyororo baridi, vituo vya huduma za mifugo 2,227, kliniki ya mifugo 27, kampuni za uagizaji chanjo 41, kampuni za utoaji huduma za mifugo 38; na
(vii) Wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa mifugo nchini.
(viii) Serikali - Kuongezeka kwa pato la taifa, kuchangia uchumi wa viwanda, kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya wananchi.

## 9.0 UZINDUZI WA KAMPENI YA CHANJO NA UTAMBUZI WA MIFUGO KITAIFA

Serikali itazindua Mpango wa Chanjo na Utambuzi wa mifugo kitaifa. Uzinduzi huu utafanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 10.0 UENDELEVU WA SHUGHULI ZA UTAMBUZI NA UCHANJAJI

Mpango huu wa chanjo unategemewa kuwa endelevu kutokana na vigezo vifuatavyo:

(i) Utekelezaji wa mpango huu utafanyika kupitia mfumo wa utawala wa Serikali uliopo ambao ni wa kudumu, aidha kila baada ya zoezi la chanjo kutakuwa kunafanyika tathmini (post vaccination evaluation) ambayo ina lengo ya kubaini ufanisi na mapungufu kwa ajili ya kuboresha utendaji katika zoezi linalofuata;

(ii) Utakuwa shirikishi, ambapo Serikali, wafugaji, watoa huduma za mifugo, wadau wa maendeleo na wataalamu wa afya ya mifugo walio nje ya mfumo rasmi wa ajira watashirikishwa katika mipango na utekelezaji wa kazi mbalimbali za mpango huu. Mpango huu utakuwa ni sehemu ya kuanzisha ajira za kudumu za wataalamu wa afya ya mifugo. Utekekezaji wa mpango kwa muda wa miaka mitano utawaunganisha wataalamu hao na utoaji wa huduma za afya kwa kuzingatia mahitaji ya soko;

(iii) Utekelezaji wa Mpango huu utatoa matokeo chanya ambayo yatabadilisha mtazamo wa wafugaji na wadau wengine kuhusiana na afya ya mifugo, jamii, biashara ya mifugo na mazao yake, kupunguzwa kwa matumizi ya dawa za matibabu na hivyo kuendelea kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake;

(iv) Wataalamu wa mifugo walioko nje ya ajira watapata fursa ya kuwaunganisha na wafugaji na hivyo kutoa fursa ya kuwa sehemu ya mfumo binafsi ambayo hautakuwa unategemea uwekezaji wa rasilimali fedha kutoka Serikalini.

## 11.0 MPANGOKAZI NA GHARAMA ZA UTEKELEZAJI WA UTAMBUZI NA UCHANJAJI

Kazi na gharama zinatakazo tumika katika utekelezaji wa mpango wa uchanjaji na utambuzi (Kiambatanisho no 1). Mpango wa utekelezaji wa kila mwaka utaandaliwa kulingana na mwaka husika.

## 10.0 UENDELEVU WA SHUGHULI ZA UTAMBUZI NA UCHANJAJI

Mpango huu wa chanjo unategemewa kuwa endelevu kutokana na vigezo vifuatavyo:

(i) Utekelezaji wa mpango huu utafanyika kupitia mfumo wa utawala wa Serikali uliopo ambao ni wa kudumu, aidha kila baada ya zoezi la chanjo kutakuwa kunafanyika tathmini (post vaccination evaluation) ambayo ina lengo ya kubaini ufanisi na mapungufu kwa ajili ya kuboresha utendaji katika zoezi linalofuata;

(ii) Utakuwa shirikishi, ambapo Serikali, wafugaji, watoa huduma za mifugo, wadau wa maendeleo na wataalamu wa afya ya mifugo walio nje ya mfumo rasmi wa ajira watashirikishwa katika mipango na utekelezaji wa kazi mbalimbali za mpango huu. Mpango huu utakuwa ni sehemu ya kuanzisha ajira za kudumu za wataalamu wa afya ya mifugo. Utekekezaji wa mpango kwa muda wa miaka mitano utawaunganisha wataalamu hao na utoaji wa huduma za afya kwa kuzingatia mahitaji ya soko;

(iii) Utekelezaji wa Mpango huu utatoa matokeo chanya ambayo yatabadilisha mtazamo wa wafugaji na wadau wengine kuhusiana na afya ya mifugo, jamii, biashara ya mifugo na mazao yake, kupunguzwa kwa matumizi ya dawa za matibabu na hivyo kuendelea kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake;

(iv) Wataalamu wa mifugo walioko nje ya ajira watapata fursa ya kuwaunganisha na wafugaji na hivyo kutoa fursa ya kuwa sehemu ya mfumo binafsi ambayo hautakuwa unategemea uwekezaji wa rasilimali fedha kutoka Serikalini.

## 11.0 MPANGOKAZI NA GHARAMA ZA UTEKELEZAJI WA UTAMBUZI NA UCHANJAJI

Kazi na gharama zinatakazo tumika katika utekelezaji wa mpango wa uchanjaji na utambuzi (Kiambatanisho no 1). Mpango wa utekelezaji wa kila mwaka utaandaliwa kulingana na mwaka husika.

**Kiambatisho 1. Gharama za Utambuzi na Utoaji chanjo kwa magonjwa ya kipaumbele kugharamiwa na Serikali kuanzia 2024/2025 - 2028/2029**

| Na | Kazi | Mk 1 (TSH) | Mk 2 (TSH) | Mk 3 (TSH) | Mk 4 (TSH) | Mk 5 (TSH) | Jumla (TSH) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | **Kuwezesha uchanjaji wa mifugo wenye tija kutoka asilimia 22 hadi kufikia zaidi aslimia 70** | | | | | | |
| 1.1 | **Kununua chanjo** | | | | | | |
| | Ugonjwa wa CBPP dozi 19097223@ 250 | 4,774,305,730 | 4,774,305,730 | 4,774,305,730 | 4,774,305,730 | 4,774,305,730 | |
| | Ugonjwa wa ND dozi 40,000,000 @ 50 | 2,000,000,000 | 2,000,000,000 | 2,000,000,000 | 2,000,000,000 | 2,000,000,000 | |
| | Ugonjwa wa PPR dozi 17,000,000 @ 250 | 4,250,000,000 | 4,250,000,000 | 4,250,000,000 | 4,250,000,000 | 4,250,000,000 | |
| | Ugonjwa wa Miguu na Midomo dozi | 0 | 1,400,000,000 | 1,400,000,000 | 1,400,000,000 | 1,400,000,000 | |
| | Ugonjwa wa kutupa mimba dozi | 0 | 300,000,000 | 300,000,000 | 300,000,000 | 300,000,000 | |
| | Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa | 0 | 1,000,000,000 | 1,000,000,000 | 1,000,000,000 | 1,000,000,000 | |
| | Ugonjwa wa mapafu ya mbuzi na kondoo (CCPP) | 0 | 3,000,000,000 | 3,000,000,000 | 3,000,000,000 | 3,000,000,000 | |
| | Ugonjwa wa Mapele ngozi | 0 | 600,000,000 | 600,000,000 | 600,000,000 | 600,000,000 | |
| | Ugonjwa wa ndigana kali (ECF) dozi | 0 | 700,000,000 | 700,000,000 | 700,000,000 | 700,000,000 | |
| ***Jumla ndogo*** | | ***11,024,305,730*** | ***18,024,305,730*** | ***18,024,305,730*** | ***18,024,305,730*** | ***18,024,305,730*** | ***83,121,528,650*** |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.2** | **Kununua Vifaa vya kutolea huduma ya chanjo** | | | | | | |
| | Cool box (@LGA =30 Pcs) | 245,250,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| | Automatic Syringes (@LGA =30 Pcs) | 294,300,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| | Needle (@LGA =300 pcs) | 16,350,000 | 0 | 0 | | | |
| | Gloves (@LGA = 10 pcs) | 19,620,000 | 19,620,000 | 19,620,000 | 19,620,000 | 19,620,000 | |
| | Overal/ overcoat (@LGA =20 pcs) | 119,900,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| | Gumboots (@LGA = 20 pcs) | 65,400,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| ***Jumla ndogo*** | | ***760,820,000*** | ***19,620,000*** | ***19,620,000*** | ***19,620,000*** | ***19,620,000*** | ***839,300,000*** |
| 1.3 | **Kuimalisha mnyoro baridi Kwenye ZVC** | | | | | | |
| | Ujenzi chumba baridi cold room ZVC Mtwara | 0 | 100,000,000 | | | | |
| | Ujenzi chumba baridi cold room ZVC Iringa | 0 | 100,000,000 | | | | |
| | Ujenzi chumba baridi cold room ZVC | 0 | 0 | 100,000,000 | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Temeke | | | | | | |
| | Ujenzi chumba baridi cold room ZVC Dodoma | 0 | 0 | 100,000,000 | | | |
| | Ujenzi chumba baridi cold room ZVC Tabora | 0 | 0 | 0 | 100,000,000 | | |
| | Ujenzi chumba baridi cold room ZVC Sumbawanga | 0 | 0 | 0 | 100,000,000 | | |
| | Ukarabati wa chumba Baridi ZVC Arusha | 0 | 0 | 0 | 0 | 100,000,000 | |
| | Ukarabati wa chumba Baridi ZVC Mwanza | 0 | 0 | 0 | 0 | 100,000,000 | |
| ***Jumla ndogo*** | | ***0*** | ***200,000,000*** | ***200,000,000*** | ***200,000,000*** | ***200,000,000*** | ***800,000,000*** |
| 1.4 | **Gharama za uchanjaji na utambuzi uwandani** | | | | | | |
| | Posho kuwezesha wataalamu uchanjaji na utambuzi | 3,405,000,000 | 3,405,000,000 | 3,405,000,000 | 3,405,000,000 | 3,405,000,000 | |
| | Posho ya mafuta kwa Halmashauri | 754,875,000 | 754,875,000 | 754,875,000 | 754,875,000 | 754,875,000 | |
| ***Jumla ndogo*** | | ***4,159,875,000*** | ***4,159,875,000*** | ***4,159,875,000*** | ***4,159,875,000*** | ***4,159,875,000*** | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.5 | **Ufuatiliaji na usimamizi** | | | | | | |
| | Ufuatiliaji na usimamizi | 953,079,135 | 953,000,000 | 953,000,000 | 953,000,000 | 953,000,000 | |
| | Usafiri (Mafuta) | 162,504,135 | 162,504,135 | 162,504,135 | 162,504,135 | 162,522,675 | |
| ***Jumla ndogo*** | | ***1,115,583,270*** | ***1,115,504,135*** | ***1,115,504,135*** | ***1,115,504,135*** | ***1,115,522,675*** | |
| 2 | **Kuimarisha usafiri wa wataalamu** | | | | | | |
| | Ununuzi wa pikipiki | 2,262,400,000 | | | | | |
| ***Jumla ndogo*** | | ***2,262,400,000*** | ***2,262,400,000*** | ***2,262,400,000*** | ***0*** | ***0*** | ***6,787,200,000*** |
| 3 | **Usanifuna ujenzi wa mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa Mifugo** | | | | | | |
| | Kusanifu na kujnga mfumo wa utambuzi | 5,000,000,000 | - | - | - | | |
| | Kununua hifadhi kuu ya taarifa (server) 3 | 75,000,000 | - | - | - | | |
| | Kununua Computer mpakato 14 | 56,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | | |
| | Kununua hereni za ng'ombe na Punda | 23,873,875,000 | 9,700,000,000 | 4,800,000,000 | 3,700,000,000 | 1,800,000,000 | |
| | Kununua hereni za mbuzi na kondoo | 17,224,200,000 | 9,125,000,000 | 6,125,000,000 | 3,250,000,000 | 1,500,000,000 | |
| | Kununua | 2,700,000,000 | - | - | - | - | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Vishikwambi | | | | | | |
| | Kutoa mafunzo tarajali ya matumizi ya mfumo kwa wataalam mbalimbali | 260,000,000 | 260,000,000 | 260,000,000 | 260,000,000 | 260,000,000 | |
| ***Jumla ndogo*** | | ***49,189,075,000*** | ***10,280,000,000*** | 19,105,000,000 | 11,205,000,000 | 7,230,000,000 | 3,560,000,000 |
| 4 | **Uanzishwaji wa maeneo huru 55 ya magonjwa ya mifugo kwa ajili ya soko la kimataifa** | | | | | | |
| 4.1 | **Uanzishwaji wa** | | | | | | |
| | Mashamba 20 ya kuku | 0 | 64,700,000 | 60,500,000 | 50,200,000 | 35,100,000 | |
| | Uanzishwaji wa mashamba 10 ya ng'ombe wa maziwa | 0 | 122,500,000 | 101,400,000 | 95,000,000 | 52,000,000 | |
| | Uanzishwaji wa mashamba 15 ya ng'ombe wa nyama | 0 | 180,000,000 | 144,000,000 | 125,000,000 | 75,000,000 | |
| | Uanzishwaji wa mashamba 15 ya mbuzi na kondoo | 0 | 120,200,000 | 100,400,000 | 82,000,000 | 53,000,000 | |
| ***Jumla ndogo*** | | 0 | 487,400,000 | 406,300,000 | 227,200,000 | 215,100,000 | 1,336,000,000 |
| 5 | **Uhamasishaji kuhusu umuhimu wa chanjo na utambuzi** | | | | | | |
| 5.1 | **Mikutano na vikao** | | | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mkutano wa wataalamu wamifugo na wafugaji nchi nzima kila Mwaka | 400,000,000 | 400,000,000 | 400,000,000 | 400,000,000 | 400,000,000 | |
| | Kutafuta na kutangaza fursa kwaenye masoko ya nje | 250,000,000 | 250,000,000 | 250,000,000 | 250,000,000 | 250,000,000 | |
| | Vyombo vya habari | 200,000,000 | 200,000,000 | 200,000,000 | 100,000,000 | 200,000,000 | |
| ***Jumla ndogo*** | | ***850,000,000*** | ***850,000,000*** | ***850,000,000*** | ***750,000,000*** | ***850,000,000*** | ***4,150,000,000*** |
| **JUMLA KUU** | | **69,362,059,000** | **37,859,704,865** | **37,819,704,865** | **35,509,304,865** | **35,589,323,405** | **216,140,097,000** |